**MTANZANIA, 18 October 2016, Page 8**

MWANZA

# Waziri ataka wawekezaji kuzingatia sheria ya mazingira

**JUDITH NYANGE Na CLARAMATIMO**

SERIKALI imejipanga kuhakikisha wawekezaji wote wa viwanda wanafanya shughuli zao nchini kwa kuzingatia sheria ya mazingira namba 20 ya mwaka 2004 na kanuni zake.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Luhanga Mpina, amesema lengo ni kulinda vyanzo vya maji na kuepusha athari za uharibifu wa mazingira.

Alikuwa akizungumza kwenye mkutano ulioandaliwa na Taasisi ya Konrad Adenauer Stiftung (KAS) kwa kushirikisha nchi za Afrika Mashariki.

> Nawaonea huruma wale ambao wamezoea kufanya kazi zao kwa mazoea bila kuzingatia sheria
>
> – Luhanga Mpina

Alisema Tanzania imewahi kulaumiwa na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA) kwa kutosimamia sheria za mazingiza hasa katika Ziwa Victoria na bunge hilo kuzitaka nchi zote kuhakikisha sheria hizo zinazingatiwa.

"Nawaonea huruma wale ambao wamezoea kufanya kazi zao kwa mazoea bila kuzingatia sheria kwa sababu wasipobadilika hawataweza kusalimika.

"Ili kuhakikisha suala hili linafanikiwa serikali itawachukulia hatua wote watakaobainika kutokuzingatia sheria hiyo ya mazingiza katika shughuli zote," alisema Mpina.

Alisema asilimia 60 mpaka 80 ya magonjwa yanatokana na athari za uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

"Kila mwaka nchi inapata hasara ya zaidi ya Sh bilionil81 kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na serikali hupoteza fedha nyingi kununulia dawa na kuwahudumia wale waliokumbwa na athari hizo," alisema.

Alisema katika kuhakikisha suala hilo linafanikiwa tayari vimefikishwa mahakamani viwanda viwili kwa kukiuka sheria za mazingira.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Utawala Bora na Demokrasia nchini ( ADLG), Jimmy Luhende, alisema ushirikishwaji wa wananchi kuhusu athari za uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi ni mdogo.

Alisema ni vema ikabuniwa namna ya kuwashirikisha wananchi moja kwa moja.